# Dar es Salaam wanaichukuliaje elimu?

## Uelewa, maoni na ushiriki wa wazazi waishio Dar es Salaam





## 1. Utangulizi

Uwazi iliyopo Twaweza, ikishirikiana na DataVision, ilifanya utafiti kuhusu hali ya utoaji wa huduma kwa wananchi mkoani Dar es Salaam katika kipindi cha Agosti na Septemba 2010. Timu iliyofanya utafiti huo ilitembelea kaya 550 katika wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni. Katika utafiti huo, kaya ziliulizwa maswali kadhaa kuhusu huduma mbalimbali za kijamii, ikiwa ni pamoja na elimu. Ili kuelewa namna wakazi wa Dar es Salaam wanavyoshiriki katika masuala ya elimu, watu waliohojiwa, wengi wao wakiwa ni wazazi, waliulizwa kuhusu uelewa wao wa sera za serikali katika elimu, maoni yao kuhusu hali ilivyo katika shule wanazosoma watoto wao, na hatua walizochukua katika kuboresha elimu katika maeneo yao.

Miongoni mwa kaya zilizohojiwa, kaya 429 zilikuwa na watoto wenye umri chini ya miaka 18. Idadi kubwa ya kaya hizo (kaya 291) zilikuwa na watoto wanaosoma katika shule za msingi, wakati kaya 152 zilikuwa na watoto wanaosoma katika shule za sekondari. Matokeo yanayowasilishwa katika muhtasari huu yanatokana na data zilizopatikana kutoka kaya zote 429 isipokuwa pale ambapo matokeo yanagusia kwa namna maalum masuala yahusuyo shule za msingi (ambapo matokeo yanatokana na zile kaya 291 zilizotajwa).

Muhtasari huu unawasilisha baadhi ya matokeo yanayotokana na utafiti huu yanayozingatia masuala ya elimu katika viwango vya shule za msingi na sekondari. Nao unaonyesha kwamba:

Uwazi pata picha kamili

Muhtasari huu umeandikwa na Kevin Croke chini ya uangalizi wa Rose Aiko, na kuchapishwa na Uwazi iliyopo Twaweza –Hivos Tanzania.

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Baruapepe: uwazi@twaweza.org.
Tovuti: www.twaweza.org/go/uwazi

Twaweza ni sisi

- Wazazi wana uelewa mdogo kuhusu vipengele muhimu vya sera ya elimu na utekelezaji wake. Karibu wazazi wote hawajui kuhusu kiasi cha ruzuku ya elimu kwa mwanafunzi ambacho serikali hupeleka mashuleni.
- Zaidi ya asilimia 80 ya wazazi hawajui kiwango cha ufaulu katika mitihani ya hivi karibuni ya kumaliza elimu ya msingi katika shule wanazosoma watoto wao.
- Wazazi wawili kati ya watano hawajui hali ya mahudhurio ya walimu katika shule wanazosoma watoto wao.
- Karibu nusu ya wazazi wamesema kwamba wanashiriki kwa kiwango fulani katika elimu ya watoto wao, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano ya kamati za shule au kwenda shuleni kuzungumza na walimu kuhusu watoto wao.
- Kwa ujumla wazazi wanaridhika na hali ya majengo ya shule; hata hivyo wachache wanaridhika na hali ya upatikanaji wa vitabu vya kiada katika shule za msingi.

Uelewa mdogo wa wazazi kuhusu masuala ya msingi katika elimu unapunguza uwezekano wa kudai ufundishaji na ujifunzaji bora zaidi kwa ajili ya watoto wao na hivyo kuzorotesha mchango wao katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

## 2. Mambo tisa kuhusu elimu Dar es Salaam


### Jambo la 1: Asilimia tisini na saba ya wazazi hawajui kiwango cha ruzuku ya elimu kwa mwanafunzi

Katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Elimu ya msingi, Tanzania imejiwekea utaratibu wa kutoa ruzuku ya elimu kwa mwanafunzi kwa shule zote ili kuongeza ubora wa elimu inayotolewa. Kwa mujibu wa sera, ruzuku hiyo ni Dola za Marekani 10 kwa kila mwanafunzi, ambazo ni sawa na Shilingi za Tanzania 15,000 kwa viwango vya kubadilishana fedha vya mwaka 2010.

Kwa kuwa fedha hizo zinalenga kutumika katika ngazi ya shule, uelewa wa wazazi kuhusu fedha hizi na ushiriki wao katika kusimamia matumizi yake kunaweza kusaidia ruzuku hii itumike vizuri. Utafiti umebaini, hata hivyo, kwamba ni asilimia 3 tu ya wazazi waliohojiwa ndio walikuwa wanafahamu kiwango cha fedha ambacho shule inapaswa kupata kwa kila mwanafunzi kupitia ruzuku hiyo. Hii ni changamoto kubwa kwa sababu kama ilivyoonyeshwa katika mihutasari yetu mingine, mara nyingi shule hazipokea ruzuku timilifu na kwa wakati. Wazazi wangejua kuhusu jambo hili wangeweza kulifuatilia ili kuhakikisha serikali inapeleka fedha hizi mashuleni kwa ukamilifu na kwa wakati. Lakini jambo hili haliwezi kufanyika ikiwa wazazi hawajui kuhusu kiasi kinachotolewa cha fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi.

Kinachovutia ni kwamba, walipoulizwa, asilimia 86 ya wahojiwa walisema wangejisikia huru kujadili kuhusu matumizi ya bajeti ya shule na mwalimu mkuu, iwapo wangeona kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Matokeo haya yanaonyesha kuwa baadhi ya wazazi wako tayari kushiriki iwapo watapatiwa fursa.

**Kielelezo cha 1: Wazazi wanaojua/ambao hawajui kiasi cha ruzuku ya elimu kwa kila mwanafunzi**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

## Jambo la 2: Licha ya kuwepo sera ya elimu ya msingi bila malipo, wazazi wameeleza kulipa ada mbalimbali

Ulipaji wa ada katika shule za serikalini umekuwa ni jambo la kawaida. Wakati ambapo kulipia gharama za mitihani ni suala la lazima, michango mingine kama vile ya ulinzi shuleni na vitabu haionekani kuendana na sera iliyopo sasa. Nusu ya wazazi wameripoti kuwa wanalazimishwa kulipa "ada ya masomo ya ziada", wakati robo ya wazazi wamesema wanalipia ada ya kawaida ya shule, hata katika shule za serikali.

**Kielelezo cha 2: Wazazi wameeleza kulipa ada katika shule za msingi za serikali**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

## Jambo la 3: Takriban asilimia 40 ya wazazi hawajui kuhusu mahudhurio ya walimu shuleni

Wazazi wameonekana kutokuwa na taarifa kuhusu mahudhurio ya walimu shuleni. Vile vile wazazi wengi wameonyesha kutokuwa na taarifa kuhusu hali ya upatikananji wa viti na huduma za vyoo katika shule wanazohudhuria watoto wao. Matokeo haya yanatofautiana na yale ya vipengele vingine kama vile ubora wa majengo, au kiwango cha elimu kwa ujumla, ambapo wazazi wachache walichagua "sijui" kama jibu lao. Matokeo yanayoonyesha ufinyu wa taarifa waliyo nayo wazazi kuhusu mahudhurio ya walimu mashuleni ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa utafiti uliofanyika hivi karibuni umeonyesha kuwa karibu asilimia 36[1] ya walimu katika maeneo ya mijini nchini Tanzania hawahudhurii shuleni. Zaidi ya hayo, ijulikane kwamba , uwepo wa mwalimu darasani ni "kiungo" muhimu sana katika mchakato wa wanafunzi kujifunza.

**Kielelezo cha 3: Vipengele vya elimu ambavyo wazazi hawajui / hawana maoni**




**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010


## Jambo la 4: Wazazi wachache sana wanajua viwango vya ufaulu katika shule wanazosoma watoto wao

Kufaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ni jambo la muhimu sana kwa wanafunzi nchini Tanzania kwa kuwa ufaulu huo ndio unaoamua iwapo watapata fursa ya kuendelea au kutoendelea na elimu ya sekondari katika shule za serikali. Kutokana na hali hii, inatarajiwa kuwa wazazi wangekuwa na hamu kubwa ya kujua kiwango cha ufaulu katika shule wanazosoma watoto wao na kufanya jitihada za kutafuta taarifa hizo. Hata hivyo, ni asilimia 18 tu ya wazazi ndio waliosema kuwa wanajua kiwango cha ufaulu katika mitihani ya karibuni katika shule wanazosoma watoto wao.

---

[1] *Service Delivery Indicators: Pilot in Education and Health Care in Africa* (2011). Washington DC: World Bank and African Economic Research Consortium. Ripoti hii inapatikana kutoka http://www.aercafrica.org/documents/isd_workingpapers/ISDReportFINAL.pdf.

**Kielelezo cha 4: Ufahamu wa wazazi kuhusu viwango vya ufaulu katika mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi katika shule wanazosoma watoto wao**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

## Jambo la 5: Wazazi wameeleza kuridhishwa na elimu inayotolewa

Asilimia 44 ya wazazi wanaridhishwa (wanaridhika au wanaridhika sana) na elimu inayotolewa katika shule za msingi, na wachache sana (asilimia 16) wanasema hawaridhiki hata kidogo. Kwa upande wa elimu ya sekondari, idadi kubwa zaidi ya wazazi (asilimia 46) walionyesha kuridhika (waliridhika au kuridhika sana) na ubora wa elimu, wakati asilimia 26 hawakuridhika au hawakuridhika hata kidogo. Takwimu zinazoripoti kiwango cha juu cha kuridhika, ikilinganishwa na viwango vya chini vya ufahamu vilivyoonyeshwa na wazazi kuhusu vipengele vya msingi vya elimu, zinavutia. Huenda kwa kiasi fulani hali hii inatokana na wazazi kuwa na matarajio ya chini au mwamko mdogo kuhusu elimu.

**Kielelezo cha 5: Viwango vya wazazi kuridhika na elimu inayotolewa katika shule za msingi na sekondari**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

## Jambo la 6: Wazazi wameonyesha kuridhishwa na majengo; wachache wanaridhishwa na hali ya upatikanaji wa vitabu

Wazazi wanaoridhishwa (wanaoridhika au wanaoridhika sana) na ubora wa elimu ya msingi inayotolewa mashuleni wanaonekana kuegemeza maoni yao hayo katika masuala kama vile ubora wa majengo. Karibu asilimia 60 ya wazazi hawa waliridhishwa na hali ya majengo ya shule. Hata hivyo, tafiti nyingine zimeonyesha kwamba upatikanaji na ubora wa miundo mbinu shuleni vina mchango mdogo katika matokeo ya ujifunzaji.[2] Wazazi wachache zaidi walionyesha maoni chanya kuhusu ubora wa walimu, moyo wa kujituma, au mahudhurio ya walimu shuleni, uwiano wa wanafunzi - mwalimu na upatikanaji wa vitabu.

**Kielelezo cha 6: Wazazi wanaoridhika au wanaoridhika sana na hali iliyopo mashuleni**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

## Jambo la 7: Nusu ya wazazi wamehudhuria mikutano ya kamati za shule katika kipindi cha miezi 12 iliyopita

Kiwango kidogo cha ufahamu kuhusu mambo kama vile ufaulu wa shule na ruzuku ya elimu kwa wanafunzi sio ishara kwamba wazazi hawana mwamko wa elimu. Karibu nusu ya wazazi (asilimia 47) wamesema kwamba walihudhuria mikutano ya kamati za shule katika shule za watoto wao angalau mara moja katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kati ya wale waliohudhuria mikutano, asilimia 61 wanaamini kwamba kamati yao ni chombo madhubuti. Hata hivyo, asilimia 24 ya wazazi hawakuwa na uhakika iwapo katika shule wanayosoma watoto wao kuna kamati ya shule.

[2] Kwa mfano tazama "Michael Kremer and Alaka Holla (2009), Improving Education in the Developing World: What Have We Learned from Randomized Evaluations", *Annual Review of Economics,* Vol 1, ukurasa wa. 513-542, pamoja na ripoti ya uchambuzi wa Uwezo 2011, "Je, watoto wetu wanajufunza*:* Kuhesabu na Kusoma katika Afrika Mashariki".

**Kielelezo cha 7: Ushiriki wa wazazi katika mikutano ya kamati za shule**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Kuhusu ushiriki rasmi katika vyombo vya usimamizi wa elimu (yaani kupitia kamati za shule), wazazi wa Dar es Salaam wanaonekana kugawanyika katika makundi matatu: washiriki wa mara kwa mara wanaosema kwamba wamehudhuria mikutano kadhaa katika kipindi cha mwaka uliopita (asilimia 19), washiriki wa mara moja moja ambao wamehudhuria angalau mkutano mmoja katika kipindi cha mwaka uliopita (asilimia 28), na wazazi wasiojishughulisha (asilimia 53) ambao wamesema hawajahudhuria mkutano hata mmoja katika miezi 12 iliyopita. Pia inaonekana wazi kwamba, kuwa na mtoto katika shule binafsi hakuongezi uwezekano wa mzazi kuhudhuria mikutano ya kamati za shule.

## Jambo la 8: Wazazi kutoka kaya zenye kipato kikubwa wanahudhuria zaidi mikutano ya shule

Uwezekano ni mkubwa zaidi kwa wazazi kutoka kaya zenye kipato cha juu kuhudhuria mikutano ya kamati za shule ikilinganishwa na wazazi kutoka kaya zenye kipato cha chini. Zaidi ya nusu ya wazazi kutoka kundi la kaya zenye kipato cha juu sana wameonyesha kuhudhuria mikutano ya kamati za shule katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti (Kielelezo cha 7). Idadi hii inapungua hadi kufikia theluthi moja ya wazazi katika makundi mawili ya chini kabisa kwa mujibu wa kiasi cha kipato.

**Kielelezo cha 8: Wazazi kutoka kaya zenye kipato cha juu wanahudhuria zaidi mikutano ya shule**





**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

**Jambo la 9: Wazazi wawili kati ya watano wameshalalamika kwa mwalimu wa mtoto wao**

Asilimia 41 ya wahojiwa wamesema kwamba walilamika wakati fulani kwa mwalimu wa mtoto wao, na asilimia 44 walikuwa na kumbukumbu ya safari ya mwisho waliyokwenda shuleni kuzungumza na walimu kuhusu mtoto wao. Kuzungumza na walimu kunaonekana kuwa jambo lenye manufaa. Kati ya wazazi 130 waliosema wamewahi kulalamika kwa walimu wa watoto wao, asilimia 72 wanaripoti kuwa wameridhishwa na namna malalamiko yao yalivyoshughulikiwa.

**Kielelezo cha 9: Wazazi waliolalamika kwa walimu kuhusu watoto wao**




**Chanzo cha data:** Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu unatoa mwanga kuhusu kiwango cha uelewa wa wazazi waishio Dar es Salaam kuhusu elimu, maoni na ushiriki wao katika elimu ya watoto wao. Muhtasari unaonyesha kuwa wazazi wana ufahamu mdogo kuhusu vipengele muhimu vya sera za elimu, ubora na utekelezaji wake. Kuhusu sera, karibu wazazi wote waliohojiwa walikuwa hawajui kiwango cha ruzuku ya elimu kwa mwanafunzi kinachotolewa na serikali mashuleni. Kuhusu ubora, zaidi ya asilimia 80 ya wazazi hawakuwa wanajua hali ya ufaulu, katika shule wanazosoma watoto wao, katika mtihani wa karibuni wa kumaliza elimu ya msingi. Zaidi ya hayo, wazazi wawili kati ya watano walionyesha kutofahamu hali ya mahudhurio ya walimu katika shule wanazosoma watoto wao. Hata hivyo, takriban nusu ya wazazi wamesema wanashiriki kwa namna fulani katika elimu ya watoto wao, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano ya kamati za shule au kwenda moja kwa moja shuleni kuzungumza na walimu kuhusu mtoto wao.

Ukweli kwamba idadi kubwa ya wazazi hawana taarifa za kina kuhusu vipengele muhimu vinavyoathiri matokeo ya ujifunzaji katika shule za watoto wao unaashiria mawasiliano duni baina ya shule na wazazi na udhaifu katika mfumo wa uwajibikaji. Wazazi wasio na taarifa za uhakika kuhusu mambo muhimu yanayoathiri shule hawawezi kudai hali bora zaidi au kuchangia kikamilifu katika kuinua ubora wa ufundishaji katika shule za watoto wao, hata kama wanahudhuria mikutano ya kamati za shule. Wanaweza kuonyesha kuridhika sana na jinsi hali ilivyo katika shule, lakini kuridhika huku kunaweza kuwa ni matokeo ya wao kutokuwa na taarifa sahihi. Iwapo ushiriki wa wazazi ni muhimu katika kuboresha ujifunzaji wa watoto, kuimarisha namna taarifa zinavyotolewa kwa wananchi na kukuza mijadala ya wananchi kunaweza kuwa mahali pazuri pa kuanzia.